# ERB-Newsletter.

Toleo Na. 008

Jarida la Mtandaoni | Juni 10, 2025



## ERB Yachagiza STEM na Kuimarisha Huduma Kanda ya Ziwa

ISSN: 000064





# WAHANDISI WATAALAM WAASWA KUSIMAMIA WAHANDISI WAHITIMU

*Mwanza - Tanzania*

▸ Na Mwandishi wetu ERB

Wahandisi wataalam wamehimizwa kuhakikisha wanatoa mwongozo kwa wahandisi wahitimu (Graduate Engineers) katika maeneo yao ya kazi ili kuwasaidia kupata uzoefu unaohitajika wa kihandisi na hatimaye kufikia usajili kama wahandisi wataalam.

Wito huo ulitolewa na Msajili Msaidizi wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Mha. Jamhuri Msabila, wakati wa hafla ya kuwaapisha wahandisi wataalam iliyofanyika Ijumaa tarehe 2 Mei 2025, jijini Mwanza. Msabila alisisitiza umuhimu wa wahandisi wataalam kufuatilia kwa makini ripoti za wahandisi wahitimu ili kuhakikisha kuwa zinakidhi viwango vya kitaaluma vinavyotakiwa na ERB.

Katika hafla hiyo, Mwanasheria wa ERB, Wakili Agricola Magera, aliwaapisha wahandisi 22 kutoka mikoa mbalimbali, hasa ya Kanda ya Ziwa. Wakili Magera alibainisha kuwa kiapo hicho kimeanzishwa chini ya Kanuni ya 4(1) ya Mwongozo wa Maadili ya Uhandisi, uliochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 278 mwaka 2014. Alitoa wito kwa wahandisi kufuata maadili ya uhandisi ili kudumisha uadilifu na ubora katika taaluma hiyo.

Aidha, Wakili Magera pia aliwaapisha wahandisi 31 wakati wa hafla ya kufunga maonyesho ya MAT BUILDERS' EXPO 2025 yaliyofanyika katika viwanja vya Samia Suluhu Hassan Bombambili mjini Geita. Maonyesho hayo yalifungwa rasmi na Msajili wa ERB, Mha. Bernard Kavishe, aliyetoa wito kwa wahandisi kuendeleza ubora wa kazi za kihandisi nchini kupitia maadili na usimamizi thabiti.

"Hafla hizi zimeonesha dhamira ya ERB katika kukuza na kudhibiti viwango vya taaluma ya uhandisi nchini, huku ikilenga kuongeza idadi ya wahandisi wataalam na kuimarisha mchango wa uhandisi katika maendeleo ya taifa." alisema Mha. Kavishe

# HATUA KWA HATUA ERB YAKAGUA UTIMAMU WA MIRADI YA UJENZI JIJINI MWANZA.

*Mwanza - Tanzania*




‣ Na Mwandishi wetu ERB

Bodi ya usajili wa wahandisi (ERB) imefanya ziara katika miradi mbalimbali inayotekelezwa katika mkoa huo.

Ukaguzi huo umeongozwa na Msajili Msaidizi wa Bodi Mha. Jamhuri Msabila, Lengo la ERB kukagua miradi hiyo imejikita kuona uzingatiaji wa matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Wahandisi Sura ya 63, katika kuhakikisha kuwa wataalam wanafanya kazi zao kwa weledi, ufanisi pamoja na kuzingatia miiko ya uhandisi.

Miongoni mwa miradi iliyokaguliwa na ERB ni pamoja na ujenzi wa majengo matano katika chuo cha DIT kampasi ya Mwanza, pamoja na ujenzi wa mradi wa kikanda wa Kituo cha Uokozi cha Kanda ya Ziwa (MRCC).

# ERB Yachagiza STEM na Kuimarisha Huduma Kanda ya Ziwa

*Geita - Tanzania*



▸ Na Mwandishi wetu ERB

Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imetekeleza mpango wake wa kuchagiza masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (STEM) katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, ikiwemo Mwanza, Geita, Mara, na Kagera, kama sehemu ya juhudi zake za kuimarisha taaluma ya uhandisi nchini.

Mkoani Geita, maafisa wa ERB wakiongozwa na Msajili wa Bodi hiyo, Mhandisi Bernard Kavishe, kwa kushirikiana na viongozi wa elimu wa Wilaya ya Geita, walitembelea shule ya sekondari ya wasichana Geita na Nyankumbu. Shule ya wasichana Geita ni moja ya shule kubwa 26 zilizoanzishwa katika kila Mkoa chini ya mpango wa Mama Samia kwa ajili ya kukuza elimu ya sayansi kwa wasichana.
Ziara hiyo ililenga kuchagiza ufundishaji na usomaji wa masomo ya STEM kwa wanafunzi wa kike huku wavulana pia wakihimizwa kushiriki kikamilifu. “Sayansi na Hisabati ndiyo mbegu inayootesha mti wa uhandisi; ndiyo msingi wa taaluma hii,” alisema Mha. Kavishe.

Kavishe alifafanua kuwa uwiano wa kijinsia katika tasnia ya uhandisi bado ni changamoto kubwa, ambapo kwa kila mhandisi mmoja wa kike, wapo wahandisi saba wa kiume. Kupitia Mpango wa STEM Support Program (SSP), ERB inalenga kufikia usawa wa kijinsia ifikapo mwaka 2030 kwa kuwahamasisha wasichana kusoma masomo ya sayansi na kuwapatia rasilimali muhimu za kujifunzia.

Katika Mkoa wa Kagera, ERB pia ilitembelea shule za sekondari Kagera River, Kyerwa, na Luteni Jenerali Silas Mayunga, huku ikikusanya rasilimali kutoka kwa wadau wa elimu na sekta binafsi kama vile Mgodi wa Dhahabu wa Geita, ili kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa STEM.

Mbali na kuchagiza STEM, ERB ilifanya ukaguzi wa wanagenzi waliopo katika Mpango wa Mafunzo Kazini (SEAP) ili kufuatilia maendeleo yao ya vitendo katika maeneo ya kazi.

Katika hatua nyingine, ERB ilihitimisha kambi yake jijini Mwanza mnamo Mei 2, 2025, kwa hafla ya kuwaapisha wahandisi wapya kama ishara ya kuwataka kutekeleza majukumu yao kwa weledi. Kambi hiyo, iliyofanyika katika ofisi za TANROADS Mwanza, ilitoa huduma mbalimbali kwa wahandisi, mafundi sanifu, na wadau wa sekta ya uhandisi.

Ziara hii imeonesha dhamira ya ERB katika kukuza vipaji vya ndani na kuimarisha usimamizi wa taaluma ya uhandisi nchini Tanzania.



# ERB KATIKA OFISI ZA MWAUWASA KUHIMIZI UZINGATIAJI WA SHERIA.

▸ Na Mwandishi wetu ERB

Bodi ya usajili wa wahandisi (ERB) imeendelea kutoa huduma kwa wakazi wa mikoa ya kanda ya ziwa,ambapo imetembelea katika ofisi za mamlaka ya maji na usafi wa mazingira (MWAUWASA) kwa lengo la kuhimiza uzingatiaji wa sheria za uhandisi hususani katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Msajili msaidizi wa ERB Jamhuri Msabila amekutana na kaimu Mkurugenzi wa kitengo cha ufundi Mhandisi Selestine Mahubi, ambaye ameeleza kwa ERB baadhi ya miradi inayotekelezwa na mamlaka hiyo ikiwemo mradi wa ujenzi wa matanki matano ya maji yenye ujazo wa lita milioni 31 miradi ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 15.









# Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita Atembelea Banda la ERB Katika Maonesho ya MAT BUILDERS' EXPO 2025

*Geita - Tanzania*

▸ Na Mwandishi wetu ERB

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Charles Chacha, alitembelea banda la Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) katika maonesho ya MAT BUILDERS' EXPO 2025 yaliyofanyika katika viwanja vya Samia Suluhu Hassan Bombambili, Manispaa ya Geita.

Katika ziara yake, Chacha aliihimiza ERB kuhakikisha inashiriki kikamilifu katika usimamizi wa miradi mikubwa inayotekelezwa mkoani Geita. Alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ubora na viwango vinavyohitajika ili kuchangia maendeleo endelevu ya mkoa huo.

Ziara hiyo ilifanyika sambamba na ufunguzi rasmi wa maonesho hayo, ambapo Chacha aliongoza hafla ya uzinduzi. Maonesho hayo yaliwaleta pamoja wadau mbalimbali wa sekta ya ujenzi na yalihitimishwa tarehe 27 Mei 2025.

Maonesho ya MAT BUILDERS' EXPO 2025 yalihudhuriwa na makampuni, wahandisi, na wadau wa sekta ya ujenzi wakionyesha teknolojia, huduma, na bidhaa zinazochochea maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini Tanzania.

# ERB Yatoa Huduma na Kuimarisha Taaluma Kanda ya Ziwa

*Mwanza - Tanzania*





▸ Na Mwandishi wetu ERB

Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) iliweka kambi yake ya huduma kwa wahandisi, mafundi sanifu, na wadau wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, iliyokuwa imewekwa katika ofisi za TANROADS jijini Mwanza. Kambi hiyo ilihitimishwa mnamo Ijumaa, Mei 2, 2025, kwa hafla ya kuwaapisha wahandisi wapya kama sehemu ya juhudi za kuimarisha maadili na weledi katika taaluma ya uhandisi.

Huduma zilizotolewa katika kambi hiyo ni pamoja na uhakiki wa usajili, malipo ya ada, usajili wa miradi, pamoja na utoaji wa elimu na taarifa mbalimbali kwa wadau. Hafla ya kiapo kwa wahandisi iliwakutanisha wataalam mbalimbali na kusisitiza umuhimu wa kufuata maadili ya uhandisi.

Katika hatua nyingine, Msajili Msaidizi wa ERB, Mhandisi Jamhuri Msabila, alitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii na Ufundi cha Misungwi kwa lengo la kupata taarifa kuhusu shughuli za chuo hicho. Akiwa chuoni hapo, Mhandisi Msabila aliwaalika watumishi wa chuo hicho kuhudhuria Mkutano wa Mafundi Sanifu (AETD), ulioratibiwa na ERB na kufanyika kati ya Mei 20 hadi Mei 22, 2025 Jijini Dar es Salaam.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Abdul Idrasa, alibainisha kuwa chuo hicho kimekuwa kikitoa mafundi sanifu wenye weledi, huku kikisimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali, ikiwemo ujenzi wa maabusu ya watoto katika Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza.

Kambi ya ERB jijini Mwanza imeonesha umuhimu wa kuwasogezea huduma wadau wa uhandisi katika maeneo yao na kujenga msingi imara wa ufanisi na maendeleo ya taaluma ya uhandisi nchini Tanzania.




# Bodi Ya Usajili Ya Wahandisi ERB Yanogesha Maonesho Ya Kimataifa Ya Wakandarasi Na Wahandisi Mkoani Geita

*Geita - Tanzania*

▸ Na Mwandishi wetu ERB

Msajili wa bodi ya usajili wa wahandisi (ERB) Mha. Bernard Kavishe amesema maonesho ya kimataifa ya Wakandarasi na wahandisi kimataifa yaliyoandaliwa na Kampuni ya MAT Builders, yaliyofanyika mkoani Geita yamekuwa fursa kwa wadau kuonesha huduma zao pamoja na kuonesha kazi za kihandisi zilizofanywa na waoneshaji kutoka katika sehemu mbalimbali duniani.

Mha. Kavishe ameyasema hayo wakati akihitimisha maonesho hayo yaliyodumu kwa siku kumi katika Viwanja Vya samia Suluhu hassan EPZ bomba mbili,Ambapo pia ERB iliweka kambi ya kutoa huduma zake kwa siku zote katika viwanja hivyo.

Msajili Kavishe pia alitumia fursa hiyo kueleza miradi mbalimbali inayotekelezwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi nchini (ERB) ikiwemo mradi wa SSP (Stem support program) ambao umelenga kuamsha hari ya wanafunzi katika shule za Sekondari kusoma masomo ya Sayansi.

" Tumeweka malengo ya kufikia usawa wa kijinsia katika uhandisi ifikapo mwaka 2030". Amesema Kavishe.

Sambamba hilo ERB pia ilitumia fursa ya maonesho hayo kutoa huduma mbali mbali kwa wahandisi na wadau, ambapo katika siku ya kufunga maonesho hayo wahandisi 31 kutoka sehemu mbalimbali ya mikoa ya kanda ya ziwa walikula kiapo ikiwa ni utayari wa kuanza kutumikia taaluma yao ramsi kwa kufata miiko ya taaluma ya kihandisi.



# BODI YA WAHARIRI




| | | |
|---|---|---|
| 1. | **Eng. Bernard Kavishe** | - Mwenyekiti |
| 2. | **Eng. Jamhuri Msabila** | - Mjumbe |
| 3. | **Eng. Veronica Ninalwo** | - Mjumbe |
| 4. | **Eng. Erick Nestory** | - Mjumbe |
| 5. | **CPA Paul Bilabaye** | - Mjumbe |
| 6. | **Adv. Mercy G. Jilala** | - Mjumbe |
| 7. | **Mr. Mariane Mgombere** | - Mhariri |
| 8. | **Mr. James Lerombo** | - Mhariri |
| 9. | **Mr. Martin Rugarabamau** | - Mhariri |
| 10. | **Ms. Wingwila Mtipa** | - Mhariri Msaidizi |
| 11. | **Mr. Mwita Nelson Chacha** | - Mhariri Mkuu |
| 12. | **Mr. Mwita Nyaimaga** | - Mbunifu Kurasa |




**ERB NEWSLETTER |** Kanda Ya Ziwa Visit

erb_tz MHANDISI TV www.erb.go.tz